JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## KUCHAPISHWA KWA WARAKA WA UGAWAJI WA MASAFA YA MAWASILIANO YA SIMU NA INTANETI KATIKA BENDI YA 3600-3800 MHz

Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172 na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306 ya Sheria za Tanzania, zinaipa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) jukumu la kupanga, kuidhinisha, kugawa, kutoa, kuchukua, kusimamisha matumizi, kufuta au kwa namna yoyote ile kurekebisha mgawo wa masafa miongoni mwa watumiaji au wamiliki wa leseni za masafa ya mawasiliano.

Mnamo tarehe 3 Februari 2025, TCRA ilitoa taarifa ya wito kwa Umma ili kutoa maoni kwenye rasimu ya Waraka wa Ugawaji wa Masafa ya Mawasiliano ya Simu na Intaneti katika bendi ya 3600-3800 MHz kwa njia ya ushindani. Wadau wa sekta ya Mawasiliano ya simu na Umma kwa ujumla walikaribishwa kuwasilisha maoni yao kwa njia ya maandishi hadi ifikapo tarehe 23 Aprili 2025. TCRA iliyapokea maoni ya wadau yaliyowasilishwa na kusasisha Waraka wa Ugawaji wa Masafa ya Mawasiliano ya Simu na Intaneti ipasavyo.

Wadau wa sekta ya Mawasiliano ya simu na Umma kwa ujumla wanataarifiwa kuwa TCRA imechapisha Waraka wa Ugawaji wa Masafa ya Mawasiliano ya Simu na Intaneti katika bendi 3600-3800 MHz na kwamba mchakato wa kuwasilisha maombi ya kushiriki kwenye zabuni ya ugawaji wa masafa kwa njia ya ushindani umefunguliwa rasmi.

Aidha, Waraka huo umeainisha taratibu mbalimbali za msingi vikiwemo vigezo vya ushiriki, sifa za mwombaji, kiwango cha juu cha masafa kinachoweza kugawiwa (Spectrum Cap) katika hatua ya awali, bei ya kuanzia ya ugawaji wa masafa (Reserve Price) na kiwango cha ulipaji kwa awamu kwa watakao shiriki na kufuzu kwenye zoezi zima la ugawaji wa masafa katika bendi 3600-3800 MHz. Waraka unapatikana katika tovuti ya TCRA kupitia **www.tcra.go.tz**.

Wadau wanasisitizwa kusoma Waraka uliochapishwa kwenye tovuti ya TCRA na kuzingatia ratiba ya zoezi la ugawaji wa masafa kwa njia ya ushindani kama ilivyooneshwa katika waraka huo.

Imetolewa Tarehe **02 Juni 2025.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Mon Jun 02 00:08:01 EAT 2025

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz